

# Kutoa ombi la kuongeza mtu mzima mtegemezi kwa usaidizi wako wa utafutaji kimbilio – orodha ya kualamisha

Oktoba 2010

Swahili

Iwapo kwa sasa unapokea usaidizi wa kimbilio (uliojulikana kama NASS) kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani (Wakala wa Mipaka wa Uingereza) na mume, mke au mwenzi wako ameungana nawe nchini Uskoti, inawezekana kuwaongeza kama wategemezi wa msaada unaopokea..

Hata hivyo, ili kuongeza mtegemezi kwa usaidizi wako wa kimbilio, Ofisi ya Nyumbani inahitaji utoe nyaraka fulani. Maombi yanayowasilishwa bila nyaraka hizi yanawezekana kutofaulu.

Unapokusanya maelezo yaliyo hapa chini, rudi ofisini mwetu katika Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti na tutapanga miadi kwa ajili yako.

Fahamu kuwa kuongeza mtegemezi kwa usaidizi wako hakumaanishi kuwa wameongezewa kwa dai lako la utafutaji kimbilio. Tungekushuri kuwa ujadiliani jambo hili na mwakilishi wako wa kisheria, kwani mabadiliko katik ahali ya jamii yako **yanaweza** kuathiri kesi yako ya uhamiaji.

## Orodha ya Nyaraka

Orodha ifuatayo itakusaidia kukusanya nyaraka zote unazohitaji kwa ombi lako. Unaporudi ofisini mwetu leta nyaraka nyingi uwezavyo kutoka kwa kila kikundi ili ombi lako liwe na nafasi nzuri ya kukubalika.

## Kimbilio

Thibitisho kuwa wewe na mwenzi wako mmeorodheshwa kwenye dai sawa la utafutaji kimbilio, kama vile:

- Nyaraka ya maelezo yoyote mapya yaliyowasilishwa kwenye Ofisi ya Nyumbani na mwakilishi wako wa kisheria yanayokuonyesha wewe au mwenzi wako kama mtegemezi wa dai la kimbilio la kila mmoja wenu.
- Nakala ya hojaji ya urithi inayoonyesha wategemezi na kuthibitisha uhusiano wenu.
- Nakala ya mahojiano yako au ya mwenzi wako ya kuchunguzwa kuhusu kila mmoja wenu.

## Uhusiano

- Iwapo umeolewa, hati yako ya ndoa.
- Iwapo hujaolewa, ushahidi wa nyaraka, kuwa wewe na mwenzi wako mume kuwa mkiishi pamoja kwa **miaka miwili ya mitatu iliyopita**, kama vile:
  - Hati za madai ya malipo katika jina zenu mbili.
  - Barua zilizotumwa kwako na kwa mwenzi wako kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani (UKBA)
  - Barua kutoka kwa mwakilishi wako wa kisheria
  - Barua kutoka kwa mtaalamu wa kimatibabu
- Nakala ya hati ya toto wako ya kuzaliwa ambayo inathibitisha kuwa wewe na mwenzi mme kuwa katika uhusinao unaoendelea kwa **miaka miwili ya mitatu iliyopita**.

## Ajira

Iwapo mwenzi wako amekuwa akifanya kazi kisheria **na** ruhusa ya Serikali ya Uingereza, lazima utoe: A written list of all previous employers, in chronological order, starting with their most recent employer

- Hati za malipo za miezi mitatu iliyopita au hati za malipo za wiki 12, pamoja na tondoti za muajiri.
- P45 yao au thibitisho lolote la kinyaraka linalothibitisha ajira imekwisha
- Nambari ya Bima ya Kitaifa
- Tarehe waliofanya kazi
- Aina ya kazi waliokuwa wakifanya

Iwapo mwenzi wako amekuwa akifany akazi bila idhini kutoka kwa Serikali ya Uingereza, lazima utoe:

- Orodha iliyoandikwa ya waajir wote wa awali, kwa njia ya wendo
- Tarehe walizofanya kazi
- Aina ya kazi waliokuwa wakifanya

Iwapo mwenzi wako **hajawahi** kufanya kazi hapo awali, lazima utoe:

- Maelezo ya jinsi wamekuwa wakijisaidia katika Uingereza
- Barua kutoka kwa marafiki wowote ambao wamewasaidia, kwa kuonyesha aina na muda wa usaidizi huo, na kueleza ni kwa nini hawawezi kutoa msaada zaidi.

### **Anwani za awali**

- Orodha iliyoandikwa ya anwani zozote za awali katika Uingereza ambapo wewe na mwenzi mliishi, kwa njia ya wendo ukianza na ya anwani mpya zaidi katika Uingereza
- Maelezo yaliyoandikwa ya mmiliki wa mali uliyouwa nayo na iwapo ulilipa chochote ili kuishi

### **Akaunti ya benki**

- Taarifa mpya za benki, zilizokamilika za miezi sita iliyopita ya akaunti **zote** za benki ulizokuwa nazo au mwenzi wako.
- Maelezo yaliyoandikwa yashughuli yoyote kubwa kama pesa kuwa kwa akaunti tofauti
- Barua kutoka kwa mtu yeyote ambaye aliweka pesa kwenye benki yako kuthibitisha kuwa waliweka pesa hizi.
- Barua kutoka kwa mtu yeyote aliyetoa pesa akithibisha kuwa alipokea pesa hizi kutoka kwako
- Barua kutoka kwa benki yako katika Uingereza ikithibitisha akaunti zozote ulizofunga

**Muhimu:** Barua utakazotoa lazima ziwe katika Kiingereza, Hata hivyo, iwapo mtu atakayetoa barua hizo hawez kuandika Kiingereza, tunapendekeza kuwa uwalete kwa miadi yako nasi ili tuweze kuwasaidia katika kuandika barua kwako.

Orodha ya anwani na maeneo ya kazi yaliyotajwa kwenye barua yanaweza kuandikwa katika lugha yako iwapo huwezi kuyaandika kwa Kiingereza.

Utakapokuja ofisini mwetu lazima ulete ushahidi wote ulioorodheshwa hapo juu ambao unahusika nawe, au hatutaweza kukusaidia na ombi lako.